
## KILIMO CHA WAKULIMA WADOGO WADOGO KINACHOZINGATIA USALAMA WA TABIANCHI

Kilimo cha wakulima wadogo wadogo kinacho zingatia usalama wa tabianchi kinahusisha njia mbalimbali za kilimo, njia ambazo huwawezesha wakulima wa jinsia zote wanaolima chini ya hekta mbili kuweza kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa chakula, maendeleo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Jambo kubwa ni kuboresha rutuba kwenye udongo na kuimarisha uhifadhi wa unyevunyevu kwenye udongo. Pia kuwahimiza wakulima kutumia njia nzuri za kilimo kama vile kupanda mbegu bora kwa umbali unao kubalika, kupunguzia miche na kung'oa magugu.

## ENEO LA MRADI

Ramani ya vijiji sita vya mradi katika wilaya ya Kilosa na Chamwino.




## UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MRADI

Mradi unafadhiliwa na kitengo cha maendeleo cha kimataifa cha nchi ya Uingereza (DfID) pamoja na wakala wa kimataifa wa maendeleo ya watu wa Denmark (DANIDA) kupitia programu ya uwajibikaji Tanzania "AcT".

Mradi huu unatekelezwa na:


actionaid
www.actionaid.org/tanzania
admin.tanzania@actionaid.org

MJUMITA (Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania): www.mjumita.org
mjumitaorg@mjumita.org

Tanzania Forest Conservation Group (Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania):
www.tfcg.org tfcg@tfcg.org

Tanzania Organic Agricultural Movement: www.kilimohai.org toam@kilimohai.org

MVIWATA (Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania): www.mviwata.org
mviwata@morogoro.net


Kwa maelezo zaidi;
Tembelea tovuti ya mradi:

www.tfcg.org/ccap.html


Au wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji, TFCG
S.L.P. 23410, Dar es Salaam
Simu:+255 22 2669007


# Mabadiliko Tabianchi, Kilimo na kuondoa Umasikini



**Kuwaweka wakulima wadogo wadogo katikati ya sera na utekelezaji wa sera yenyewe**

## MABADILIKO TABIANCHI NA WAKULIMA WADOGO WADOGO TANZANIA.

Wakulima wadogo wadogo wanatakiwa kupewa kipaumbele katika sera na katika utekelezaji wa sera za Tanzania ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kilimo ni njia kuu ya Tanzania kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

Wakulima wadogo wadogo wataathirika/ wanaadhirika zaidi na adhari za mabadiliko tabianchi.

Mabadiliko ya matumizi ya ardhi, hasa ufyekaji wa misitu utokanao na kilimo cha kuhamahama, ni chanzo kikubwa cha uzalishaji wa hewa ukaa Tanzania.

Sera na kanuni za uwekezaji na kilimo vinatoa kipaumbele kwa kilimo kikubwa cha kutumia mashine zenye kutumia nishati ya mafuta na chenye lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza masoko ya mazao. Wakati njia hii inaweza kuongeza uzalishaji kwa kipindi kifupi, pia inaongeza uwezekano wa wakulima wadogo wadogo kuwa masikini na kuathiriwa zaidi na mabadiliko tabianchi yanayotokana na ongezeko la hewa ukaa itokanayo na matumizi tegemezi ya nishati ya mafuta, sambamba na kuongezeka kwa uharibifu wa misitu kwenye maeneo ya wakulima wadogo wadogo waliohamishwa kupisha wakulima wakubwa na kwenye ufunguzi wa mashamba mapya.

Tanzania ipo hatarini kushindwa kupambana na mabadiliko tabianchi hasa katika sekta ya kilimo.

Mabadiliko tabianchi kwa sasa kama vile ukame na mafuriko, tayari yamesababisha gharama kubwa za kiuchumi Tanzania. Kwa mwaka matukio hayo hugharimu zaidi ya asilimia moja ya pato la taifa na yamekua yakitokea mara kwa mara, hivyo hupunguza malengo marefu ya ukuaji wa uchumi na kuadhiri maisha ya mamilion ya watu (Uchumi wa Mabadiliko Tabianchi , DfID 2011).

## MRADI

### Maelezo ya jumla ya Mradi

Mradi huu ni wa ubia kati ya mashirika matano yasiyo ya kiserikali.Unahusisha uraghibishi katika ngazi ya taifa na maonyesho ya njia mbalimbali za kilimo hifadhi ndani ya vijiji vitatu vilivyo ukanda wa ukame katika wilaya ya Chamwino na vijiji vitatu vilivyopo maeneo ya milimani katika wilaya ya Kilosa. Mradi umeanza Octoba 2012 na utakwisha Disemba 2014.

### Lengo la Mradi

Lengo la mradi ni kupunguza umasikini miongoni mwa wakulima wadogo Tanzania na kuwajengea uwezo wa kukabiliana na mabadiliko tabianchi ikiwa ni pamoja na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kwa kuboresha njia za kilimo.

## SHUGHULI ZA MRADI

Ili kufikia lengo la mradi, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

- ✓ Kujenga uwezo wa wanachama na watumishi wa mitandao ya kitaifa ya vikundi vya wakulima wadogo wadogo Tanzania (MVIWATA) na mtandao wa jamii wa usimamizi misitu Tanzania (MJUMITA) kushirikiana kikamilifu kuhimiza kilimo cha wakulima wadogo wadogo kinachozingatia usalama wa tabianchi.
- ✓ Tafiti za njia bora juu ya kilimo cha wakulima wadogo wadogo kinachozingatia usalama wa tabianchi Tanzania.
- ✓ Kujengea uwezo wakulima katika vijiji sita kutekeleza na kuonyesha kwa vitendo kilimo kinacho zingatia usalama wa tabianchi.
- ✓ kutumia vyombo vya habari na kushirikiana na viongozi wa kuchaguliwa kuweza kuhamasisha uundwaji na utekelezaji wa sera zinazosaidia kilimo kinachozingatia usalama wa tabianchi.







